



## Aina ya miti Toleo TTS13

### Mhoba

*Cassia spectabilis*, (Family Leguminosae, subfamily Caesalpinaceae)

Mwenu ni mti wa kimo cha kadri na shina la rangi ya kijivu. Mti huu haushambuliwi na mchwa na hupandwa kurembesha mazingira. Mti huu waweza kuchangia viwango vya Nitrogen kwenye mchanga.

**Majina mengine:** *Cassia humboldtiana*, *Cassia speciosa*, *Pseudocassia spectabilis*, *Senna spectabilis*.

**Majina ya kawaida:** Cassia, mwenu, mhomba, antsoan dilaw, *scented shower*.

**Maenezi:** Mti huu ulitokea sehemu ya Amerika ya Kati na upande wa Kaskazini mwa Amerika ya Kusini. Mti huu umesambaa katika Afrika, ikiwemo, Angola, Burindi, Afrika Kusini na Afrika ya Mashariki

### Mazingira

Mvua: 800-2000mm, hata hivyo viwango vya 100-3000mm vimerekodiwa Nchini Ufilipino.

Kiwango cha joto: 14-32°C.

Muinuko: 0-2000m.

Aina ya mchanga: Mchanga ulio na unyevunyevu na hata mchanga ulio na changarawe.

### Maumbile

Urefu: 10-12m na hata kufikia 20m.

Sehemu ya juu: Matawi husambaa.

Maua: Maua ya rangi ya manjano hujitokeza mwishoni mwa msimu wa joto.

Matunda: Tunda refu la kijani kibichi na kubadilika kwa rangi nyeusi.

### Matumizi

Matumizi ya maana: Kama kivuli, kuzuia upepo, kuimarisha rutuba, kama boji, kuni na useremala.

Matumizi mengine: Maua husaidia nyuki na pia mti huu hutumiwa kama kivuli.



## **Maelezo ya upanzi**

Wawezakupanda mwenu kwa kutumia mbegu au vipandikizi.

Mbegu: Kuna takriban mbegu 39000 kwa kilo. Mbegu zaweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu.

Utaratibu wa kupanda mbegu: Weka mbegu kwa maji moto kwa muda mfupi kisha kuloweka kwa saa 24.

Kumea: Waweza kupata asilimia ya 60-90%.

Utunzaji: Kukata au kupogoa mizizi huhitajika kufanywa mara kwa mara.

## **Majulisho**

Makala haya yametafsiriwa na:

**Centre For Natural Resource Management, Advocacy And Marketing (Cream)  
P.O Box 1427,  
50300-Maragoli.  
Kenya.**

E-mail: [cream-creamorg@excite.com](mailto:cream-creamorg@excite.com)

---

**HDRA**- Kwa huduma za kilimo hai, Ryton Organic Gardens Coventry, CV8 3LG, UK  
Simu +44 (0)24 7630 3517 Kipepesi +44 (0)24 7663 9229 Barua pepe: [ove-enquiry@hdra.org.uk](mailto:ove-enquiry@hdra.org.uk)  
Mtandao: <http://www.hdra.org.uk>

Makala haya ni mkusanyiko wa utafiti wa kisayansi na maarifa ya kilimo hai. Maelezo ya ziada kuhusu mbinu za kilimo hai yaweza kupatikana kutoka kwa HDRA. Waweza kunakili makala haya kwa sababu zisizo za kifaida.

This update: Feb 2005